SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

MHESHIMIWA ISSA HAJI USSI GAVU

KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA

2017/2018

Mei, 2017

YALIYOMO ii
ORODHA YA VIAMBATISHO iii
VIFUPISHO VYA MANENO iv
1. UTANGULIZI 1
2. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2016/2017 3
2.1 MAFANIKIO YA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2016/2017 4
3. MWELEKEO WA BAJETI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 28
3.1 PROGRAMU KUBWA NA NDOGO NA MAKISIO YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 30
4. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 39
4.1 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MRADI WA MAENDELEO 39
4.2 MAOMBI YA FEDHA 2017/2018 39
5. HITIMISHO 40

ORODHA YA VIAMBATISHO

KIAMBATISHO 1: ORODHA YA WAGENI WALIOFIKA IKULU KUONANA NA MHESHIMIWA RAIS 42

KIAMBATISHO 2: MAPITIO YA UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 44

KIAMBATISHO 3: MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 46

KIAMBATISHO 4: MAFUNZO YA MUDA MREFU KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2016/2017 48

KIAMBATISHO 5: IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOENDA LIKIZO KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI, 2016/2017 49

KIAMBATISHO 6: ORODHA YA NYARAKA ZA SERA NA SHERIA ZILIZOJADILIWA NA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2016/2017 50

KIAMBATISHO 7: IDADI YA WATUMISHI WALIOFANYIWA UPEKUZI NA TAASISI WANAZOTOKA 51

VIFUPISHO VYA MANENO

ACGN	Africa Cabinet Government Network
AfDB	African Development Bank
CCM	Chama cha Mapinduzi
COMESA	Common Market for Eastern and Southern Africa
CPC	Communist Party of China
Dk.	Daktari
EAC	East African Community
EPA	Economic Partnership Agreement
IGAD	Intergorvenmental Authority on Development
IORA	Indian Ocean Rim Association
MKUZA	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar
MoU	Momerandum of Understanding
OMPR	Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais
ORMBLM	Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
PBB	Program Based Budget
SADC	Southern African Development Community
SMT	Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
SMZ	Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TZS	Tanzania Shillings
UKIMWI	Ukosefu wa Kinga Mwilini
UN	United Nation
UNDP	United Nation Development Program
VVU	Virusi Vya Ukimwi

1. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu, likae kama Kamati kwa ajili ya kupokea, kujadili, kuzingatia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Kazi za Maendeleo ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa Fedha 2017/2018.

2. **Mheshimiwa Spika,** naanza hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wenye afya njema. Aidha, namshukuru kwa kunipa nguvu ya kuweza kuwasilisha hotuba ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa Fedha 2017/2018.

3. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutumia fursa hii adhimu kwa namna ya kipekee kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa imani yake kwangu kwa dhamana na majukumu aliyonikabidhi, naomba nimuahidi kuendelea kutumia uwezo wangu wote katika kufanya kazi kwa bidii na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

4. **Mheshimiwa Spika,** naomba niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuongoza vyema na kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020. Hali hii inapelekea kufikiwa kwa ahadi alizoahidi kuzitekeleza wakati akiomba ridhaa ya Wananchi kuiongoza Zanzibar kwa kipindi cha pili cha Awamu ya Saba. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu, afya njema na maisha marefu yeye na familia

yake ili aweze kuyatekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

5. **Mheshimiwa Spika,** nakupongeza wewe binafsi, Naibu wako Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Wenyeviti Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Mheshimiwa Shehe Hamad Mattar kwa kuliongoza vizuri Baraza letu. Umahiri wako katika kutuongoza unapelekea kuwa na mijadala iliyowazi na huru kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu. Hali hii inapelekea kukua kwa Demokrasia ndani ya chombo hiki cha kutunga Sheria na kupatikana kwa Sheria zinazoakisi maisha ya Wananchi.

6. **Mheshimiwa Spika,** shukrani maalum ziende kwa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Omar Seif Abeid, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Konde. Kamati hii imekuwa ikitoa ushirikiano mkubwa kwa Ofisi yetu. Aidha, inatupatia miongozo, ushauri na maelekezo ambayo yanapelekea kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Naiomba Kamati iendelee kushirikiana na kushauriana na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kutekeleza wajibu wake. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inaahidi kuendeleza ushirikiano mwema uliopo na tunaahidi kuyafanyia kazi yote watakayotuelekeza.

7. **Mheshimiwa Spika,** kabla sijamaliza salamu zangu za pongezi, kwa heshima kubwa napenda kutoa pongezi kwa Wananchi wa Zanzibar kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali yao katika jitihada zake za kuwaletea maendeleo. Nawaomba waendelee kudumisha amani, umoja na mshikamano tulionao ambao ndio nguzo ya maendeleo yetu. Aidha, nawashukuru Wananchi wenzangu wa Jimbo

letu la Chwaka kwa mashirikiano wanayonipatia. Naahidi kuendelea kuwatumikia kwa moyo na nguvu zangu zote na nitaendelea kuzitekeleza ahadi nilizozitoa, kama nilivyoahidi.

8. **Mheshimiwa Spika,** kama tunavyojua Nchi yetu ipo katika kipindi cha mvua za masika na baadhi ya Wananchi wamepata athari kutokana na mvua hizo. Tunawapa pole Wananchi wenzetu waliopata athari za maporomoko ya ardhi hasa katika maeneo ya Mkoa wa Kusini Pemba. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie mvua hizi ziwe zenye neema, baraka na atuepushe na mitihani. Natoa wito kwa Wananchi wazitumie vizuri mvua hizi ikiwemo kupanda mazao ya chakula na biashara. Aidha, nawaomba wachukue tahadhari kwa kuweka mazingira safi ili wajiepushe na uwezekano wa kutokea maradhi ya mripuko kama kipindupindu.

9. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba uniruhusu niwasilishe kwa ufupi Utekelezaji wa Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha Julai – Machi 2016/2017.

2. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2016/2017

10. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilitengewa jumla ya TZS. 6,990.2 milioni kwa Fungu A01 na A02. Fungu A01 lilitengewa jumla ya TZS. 5,498.2 milioni. Kati ya hizo TZS. 500.0 milioni kwa ajili ya mradi wa maendeleo na TZS. 4,998.2 milioni kwa ajili ya kazi za kawaida na Fungu A02 lilitengewa jumla ya TZS. 1,492.0 milioni. Hadi

kufikia mwezi Machi, 2017 Fungu A01 liliingiziwa jumla ya TZS. 3,742.8 milioni. Kati ya hizo TZS. 500 milioni kwa ajili ya mradi wa maendeleo na TZS. 3, 611.8 milioni kwa ajili ya kazi za kawaida na Fungu A02 liliingiziwa jumla ya TZS. 980.2 milioni.

11. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilitekeleza Programu kuu tano na ndogo 14 chini ya Mafungu mawili ambayo ni A01 na A02. Utekelezaji wa Programu hizi, ulizingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020, MKUZA II, Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa katika ufunguzi wa Baraza la Tisa la Wawakilishi pamoja na miongozo, maelekezo na maagizo yanayotolewa kwetu. Kupitia Programu zake, Ofisi iliandaa Mpango Kazi wa mwaka 2016/2017 na kuweka vipaumbele katika maeneo yafuatayo:-

i. Kuimarisha Utendaji wa Serikali;
ii. Kuwaunganisha Wananchi wa Zanzibar;
iii. Mambo ya Nje na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC); na
iv. Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi.

2.1 MAFANIKIO YA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2016/2017

12. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 lilipata mafanikio ya kuridhisha kupitia Programu zake kama ifuatavyo:-

Programu ya Kusimamia shughuli za Mheshmiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu

13. **Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuona kuwa Umma na Washirika wote kwa ujumla wanakuwa na uelewa mzuri kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Serikali yao. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii iliidhinishiwa TZS. 2,867.4 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 iliingiziwa TZS. 2,066.4 milioni sawa na asilimia 87 kwa kazi za kawaida na TZS. 500.0 milioni sawa na asilimia 100 kwa kazi za maendeleo.

14. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii mafanikio makubwa yamepatikana yakiwemo kuongezeka kwa uelewa wa Wananchi baada ya Ofisi kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo na kijamii kupitia Jarida la Ikulu na vipindi vinavoandaliwa na kurushwa hewani kupitia vyombo vya habari. Aidha, ziara zinazofanywa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ndani na nje ya Nchi zimewawezesha Wananchi kujua utekelezaji halisi unaofanywa na Serikali.

15. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alifanya ziara mbili za kikazi nje ya Nchi. Ziara ya kwanza alimuwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dk. John Pombe Joseph Magufuli, katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi, (IORA), uliofanyika Jakarta, Indonesia tarehe 5 hadi tarehe 7 Machi, 2017. Aidha, alifanya Ziara ya Kiserikali Nchini Djibouti kuanzia tarehe 07 hadi tarehe 9 Mei, 2017.

16. **Mheshimiwa Spika,** katika mkutano wa Viongozi wa IORA, Mheshimiwa Rais aliongoza ujumbe wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliowajumuisha Waheshimiwa Mawaziri, Mshauri wa Rais na Watendaji wengine wa Serikali zote mbili. Mkutano huo uliofunguliwa na Mheshimiwa Joko Widodo, Rais wa Indonesia, ulitanguliwa na Mkutano wa Maafisa Waandamizi na Mkutano wa Baraza la Mawaziri. Vile vile, palifanyika Mkutano wa Baraza la Wafanyabiashara uliozikutanisha Taasisi mbali mbali za kibiashara.

17. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali Wanachama wa IORA, ulipitia taarifa za Mkutano wa Baraza la Mawaziri na Mkutano wa Masuala ya Biashara ikiwemo makubaliano ya IORA, yaitwayo "Jakarta Concord" yenye maeneo sita ambayo ni Biashara; Uvuvi; Menejimenti ya Udhibiti wa Majanga; Taaluma, Sayansi na Teknolojia; Utalii na Utamaduni.

18. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano huo uliridhia Mpango wa Makubaliano ya Jakarta (Concord) ambapo ulitiwa saini lakini pia mkutano huo ulipitisha Mpangokazi wa Mkataba huo wa muda wa miaka mitano (2017-2021). Kadhalika, mkutano ulipitisha Azimio la Kukabiliana na Vitendo vya Ugaidi na Misimamo Mikali. Taarifa inayohusu Uvumbuzi na Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi nayo ilipokelewa. Viongozi walipata fursa ya kutoa Hotuba fupi ambazo zilisisitiza juu ya Mabadiliko ya Tabia Nchi, Umuhimu wa Majadiliano, Kudumisha Mashirikiano baina ya Nchi Wanachama pamoja na Kuimarisha Miundombinu. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imependekeza isimamie eneo la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi.

19. **Mheshimiwa Spika,** wakati akiwa Nchini Indonesia, Mheshimiwa Rais alionana na kufanya mazungumzo na Makamo wa Rais wa Nchi hiyo, Mheshimiwa Muhammad Jusuph Kalla, tarehe 8 Machi, 2017. Katika mazungumzo yao, viongozi hao walikubaliana kudumisha na kuimarisha ushirikiano wa kihistoria uliopo baina ya Indonesia na Zanzibar na Tanzania nzima kwa ujumla. Mheshimiwa Rais, aliwakaribisha Wawekezaji kutoka Indonesia kuja kuwekeza Tanzania katika Sekta ya Viwanda na nyenginezo. Alishauri ushirikiano wa muda mrefu uendelezwe, katika Nyanja ya Utafiti, utoaji wa Mafunzo na kubadilishana wataalamu. Makamo wa Rais wa Indonesia aliisifia Zanzibar kwa uzalishaji wa Karafuu zenye sifa ya pekee Duniani. Aliunga mkono ushirikiano katika Sekta ya Kilimo na nyenginezo. Kadhalika, viongozi hao walikubaliana juu ya haja ya kukuza utalii na kupanua ushirikiano katika nyanja mpya zikiwemo safari za ndege na sekta ya Mafuta na Gesi.

20. **Mheshimiwa Spika,** ziara ya pili ya Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ilikuwa katika Jamhuri ya Djibouti tarehe 7 hadi 9 Mei, 2017, kufuatia mualiko wa Rais wa nchi hiyo, Mheshimiwa Omar Ismail Guelleh. Ziara hiyo ilikuwa na lengo la kuanzisha uhusiano na ushirikiano baina ya nchi zetu mbili. Wakati akiwa nchini humo, Mheshimiwa Rais alikutana na kufanya mazungumzo na Mheshimiwa Rais Geulleh ambapo Viongozi hao wawili walikubaliana kuanzisha uhusiano na ushirikiano hasa katika sekta za jamii, maendeleo na uchumi kwa manufaa ya pande zote mbili.

21. **Mheshimiwa Spika,** maeneo yaliyotiliwa mkazo katika uhusiano huo ni Miundombinu na Mawasiliano; Usafiri, Usafirishaji na Utalii; Biashara na Uwekezaji; Shughuli za Bandari; Shughuli za Maeneo Huru ya Kiuchumi, Uvuvi pamoja na Kutembeleana baina yetu kwa lengo la kubadilishana uzoefu. Kadhalika, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Ismail Omar Guelleh waliarifiwa juu ya mazungumzo ya Waheshimiwa Mawaziri wa pande mbili yaliyofanyika hapo kabla, wakati wa ziara hiyo. Kutokana na mazungumzo hayo, iliandaliwa taarifa ya pamoja (Communique) ambayo itatumika katika utekelezaji wa uhusiano na ushirikiano wa pande mbili.

23. **Mheshimiwa Spika,** ziara ya Mheshmiwa Rais nchini Djibouti ilikuwa ya mafanikio kwani imefungua milango ya uhusiano na ushirikiano baina ya nchi mbili hizi. Jamhuri ya Djibouti inategemea kufaidika kwa kujifunza mengi kutoka Zanzibar katika Sekta ya Utalii na nyenginezo, wakati Zanzibar itafaidika katika nyanja za Uwekezaji, Mawasiliano, Bandari na sekta nyenginezo.

24. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa Mheshimiwa Rais alikuwa Mgeni rasmi katika kilele cha sherehe za Mbio za Mwenge zilizofanyika katika viwanja vya Halmashauri ya Bariadi, Mkoa wa Simiyu tarehe 15 Oktoba, 2016. Katika hotuba yake aliyoitoa siku hiyo, pamoja na mambo mengine, alielezea juhudi zinazochukuliwa na Serikali zote mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukuza ajira kwa vijana na kuwataka vijana kuchangamkia fursa hiyo na kuimarisha uzalendo.

25. **Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Rais aliendelea kushiriki katika shughuli mbali mbali za maendeleo ikiwa pamoja na ufunguzi wa jengo la Mahakama Kuu liliyoko Chake Chake Pemba uliofanyika tarehe 06 Novemba, 2016. Aidha, Mheshimiwa Rais alizindua majengo mapya ya Wodi ya Kinamama na Watoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja uliofanyika tarehe 11 Novemba, 2016. Vile vile, katika kuhakikisha kuwa Wananchi wa Pemba wanapata huduma za Afya zilizo bora na karibu na maeneo wanayoishi, tarehe 26 Novemba, 2016, Mheshimiwa Rais alifungua Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani baada ya kujengwa upya.

26. **Mheshimiwa Spika,** katika kuadhimisha sherehe za miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alijumuika na Wananchi kuzindua miradi ya maendeleo ikiwemo ufunguzi wa Kiwanda cha Maziwa cha Azam Marine Diary kinachomilikiwa na Kampuni ya Bakhresa kilichopo Fumba tarehe 5 Januari, 2017. Aidha, alishiriki katika ufunguzi wa Majaribio ya Mkakati wa Tasnia Malibunifu (Branding) Saateni na uwekaji wa Jiwe la Msingi la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu iliyopo Mazizini tarehe 6 Januari, 2017.

27. **Mheshimiwa Spika,** katika muendelezo wa Sherehe hizo, tarehe 07 Januari, 2017 Mheshimiwa Rais alifungua Skuli ya Sekondari ya Mohamed Juma Pindua ya Mkanyageni. Vile vile, Mheshimiwa Rais alifungua Soko la Wete pamoja na Ofisi ya Baraza la Mji tarehe 08 Januari, 2017. Mheshimiwa Rais alikuwa Mgeni rasmi katika hafla ya uwekaji wa Jiwe la Msingi la Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi katika eneo la Fumba tarehe 9 Januari, 2017. Aidha, tarehe 11 Januari, 2017 alifungua Ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Kwarara na Kituo cha Matangazo ya Elimu.

28. **Mheshimiwa Spika,** shughuli nyengine alizofanya Mheshimiwa Rais katika kuendeleza na kukuza tasnia ya michezo na vipaji, alikabidhi vifaa vya michezo kwa ajili ya maandilizi ya timu 18 za Mpira wa Miguu za Majimbo ya Unguja ili kushiriki vizuri katika michuano ya Ligi za Majimbo tarehe 26 Februari, 2017. Shughuli kama hiyo ameifanya katika Majimbo ya Pemba tarehe 17 Machi, 2017. Aidha, katika kuendeleza utaratibu wake wa kuzungumza na vyombo vya habari kwa lengo la kuimarisha Uwazi na Uwajibikaji pamoja na Utawala Bora, tarehe 23 Machi, 2017 Mheshimiwa Rais aliwaita waandishi wa habari wa vyombo mbali mbali vya Tanzania na aliwapa fursa wamuulize masuala kuhusiana na mipango pamoja na utekelezaji wa mambo mbali mbali katika sekta zote za Kiuchumi na Kijamii.

29. **Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 28 Machi, 2017, Mheshimiwa Rais alifanya mkutano na walimu wa skuli za Sekondari za Unguja na tarehe 6 Aprili, 2017 alifanya mkutano kama huo kwa upande wa Pemba. Katika mikutano hiyo, Mheshimiwa Rais aliwaeleza walimu hao, kwamba Serikali itaendeleza juhudi zake za kuimarisha sekta ya elimu nchini na aliwataka walimu wa Sekondari wazidishe uwajibikaji kwa kuzingatia ubora na umuhimu wa elimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

30. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, Mheshimiwa Rais alikuwa mgeni rasmi katika Sherehe za Uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017, zilizofanyika katika uwanja wa Kumbukumbu Mjini Mpanda, Mkoani Katavi tarehe 02 Aprili, 2017. Katika sherehe hizo, Mheshimiwa Rais aliwakilishwa na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais alisisitiza juu ya umuhimu wa kuimarisha

mashirikiano baina ya Serikali zetu mbili, wafanyabiashara na wawekezaji wa Ndani na Nje ya Nchi katika kuijenga Tanzania yenye viwanda kwa lengo la kukuza ajira na kuwa na matumizi bora ya rasilimali zetu.

31. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 01 Mei, 2017, Mheshimiwa Rais aliongoza wafanyakazi na wananchi katika Sherehe za Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, Mei Mosi, zilizofanyika katika Mkoa wa Kaskazini, Wilaya ya Kaskazini "B", Unguja kwenye Viwanja vya Polisi Mahonda. Katika sherehe hizo, Mheshimiwa Rais alisisitiza juu ya suala la uwajibikaji kwa wafanyakazi, ikiwa ndio msingi wa maendeleo yetu. Alisema kuwa kwa upande wa Serikali itaendelea na utaratibu wake wa kuzilinda haki zote za wafanyakazi na kuimarisha maslahi yao hatua kwa hatua. Hivyo, Mheshimiwa Rais aliwahimiza viongozi wote walioteuliwa na waliochaguliwa na wananchi kuwa wabunifu na makini katika kusimamia majukumu waliyopewa na kuwahudumia wananchi ipasavyo. Kadhalika, Mheshimiwa Rais aliwataka Viongozi wote watekeleze wajibu wao kwa kuwasimamia wafanyakazi wanaowaongoza pamoja na wao wenyewe watekeleze vyema majukumu waliyopangiwa. Kwa upande wao, Uongozi wa Chama cha Wafanyakazi ulimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutimiza ahadi yake ya kupandisha kima cha chini mshahara kutoka TZS. 150,000 hadi TZS. 300,000.

32. **Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikutana na wageni mbali mbali wakiwemo Mawaziri, Viongozi wa Serikali wa SMT, Mabalozi, Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa, Viongozi wa Dini, Wafanyabiashara na Wawekezaji. Viongozi hao walizungumza kuhusu mashirikiano baina ya Tanzania na Nchi zao na Zanzibar na kuimarisha uhusiano wa Biashara, Utalii na Uwekezaji.

33. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 01 Machi, 2017, Mheshimiwa Rais alikutana na ujumbe wa Wakurugenzi Watendaji 12 wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) wanaofanyia kazi zao ndani na nje ya Bara la Afrika. Wakurugenzi hao kwa pamoja walimpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais, kwa uongozi wake mahiri uliopelekea kuimarika kwa uchumi wa Zanzibar na kuahidi kwamba Benki hiyo itaendelea kuisaidia na kuiunga mkono Zanzibar, katika juhudi zake za kuimarisha uchumi wake na kukuza sekta mbali mbali za Kijamii na Maendeleo.

34. **Mheshimiwa Spika,** Ujumbe wa watu 12 wa Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) ulitembelea Zanzibar tarehe 23 Machi, 2017 na kuonana na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ujumbe huo uliongozwa na Mheshimiwa Guo Jinlong – Mjumbe wa Kamati Kuu na Katibu wa Kamati ya Chama cha Kikomunisti cha Manispaa ya Beijing. Wakati wa mazungumzo yao, Viongozi hao walisisitiza kuendeleza ushirikiano na uhusiano wa kirafiki uliopo baina ya Zanzibar na Jamhuri ya Watu wa China. Kadhalika, Mheshimiwa Guo Jinlong alimuhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China itatekeleza ahadi yake ya kumalizia ujenzi wa Jengo la Abiria (terminal III) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

35. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 11 Aprili, 2017, Mheshimiwa Rais alikutana na ujumbe wa Wawakilishi 23 wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN) waliopo Tanzania. Ujumbe huo uliongozwa na Mwakilishi Mkaazi wa Umoja wa Mataifa Nchini Tanzania ambae pia ni Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) Nchini Tanzania Bwana Alvaro Rodriguez. Katika mazungumzo yao, ujumbe huo ulisisitiza azma ya Umoja wa Mataifa

kuendelea kuisaidia na kuiunga mkono Zanzibar katika nyanja mbali mbali. Orodha kamili ya wageni aliokutana nao Mheshimiwa Rais inaonekana kiambatisho Nam. 1.

36. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Faragha ya Rais kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imefuatilia maagizo 617 na ahadi 12 za Mheshimiwa Rais ambazo ziko katika Sekta za miundombinu, afya, elimu na ustawi wa jamii katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba, jambo ambalo limesaidia kwa kiasi kikubwa kupatikana kwa ufumbuzi wa changamoto kadhaa zinazowakabili Wananchi.

37. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Faragha ya Rais imewaendeleza wafanyakazi wake katika fani mbali mbali. Ofisa mmoja anaendelea na mafunzo yake ya Shahada ya Uzamivu katika fani ya lugha ya Kiswahili kwenye Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na mwengine ameanza masomo yake ya Shahada ya Uzamivu, katika fani ya Sheria za Kimataifa Nchini China. Aidha, Ofisa mmoja alihudhuria katika masomo ya muda mfupi ya Hoteli na Ukarimu Nchini China. Wakati huo huo, Wafanyakazi wengine wawili walihudhuria mafunzo ya muda mfupi ya Hoteli na Ukarimu Nchini India na mfanyakazi mmoja anaendelea na masomo ya muda mrefu katika fani hiyo, katika ngazi ya Stashahada kwenye Taasisi ya Utalii, Maruhubi. Vile vile, Mfanyakazi mmoja alihudhuria mafunzo ya muda mfupi ya Ukutubi katika Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji Mkoani Mbeya.

38. **Mheshimiwa Spika,** mbali na majukumu yaliyoainishwa, Ofisi imeweza kutekeleza kazi mbali mbali zikiwemo kutoa huduma kwa wageni wanaoalikwa na Mheshimiwa Rais. Majukumu mengine yaliyotekelezwa ni kutunza na kutoa huduma katika majengo ya Ikulu ya Mnazi Mmoja, Ikulu ndogo ya Migombani, Ikulu ya Mkoani, Chake Chake,

Kibweni, Nyumba ya Rais wa Zanzibar iliyopo Dar es Salaam (Laibon) na Dodoma.

39. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Faragha ya Rais inaendelea na ujenzi katika Ikulu ya Micheweni na Chake Chake. Ikulu ya Bwefum na Nyumba ya Rais wa Zanzibar iliyopo Dar es Salaam (Laibon) zimezungushiwa uzio ili kuimarisha ulinzi. Aidha, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara imepewa kazi ya kuzuia mmong'onyoko wa udongo katika Ikulu ya Mkoani.

40. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mawasiliano na Habari – Ikulu imetayarisha vipindi 24 Vya radio na televisheni na kurushwa hewani kupitia vituo vya Redio na TV. Vipindi hivi viliandaliwa kwa madhumuni ya kuwapa habari sahihi Wananchi juu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM 2015 – 2020. Ili kwenda sambamba na Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, Idara imeendelea kutoa taarifa kupitia Tovuti ya Ikulu www.ikuluzanzibar.go.tz pamoja na Mitandao ya Kijamii na "live stream".

41. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeendelea kuwapa taarifa Wananchi kupitia jarida la Ikulu ambalo limekuwa likichapishwa kila mwezi. Jarida hili linaelezea kwa kina utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na kutoa fursa kwa Wananchi kutoa maoni yao kuhusiana na utekelezaji wa Miradi hiyo. Vile vile, Idara imechapisha kalenda 5,500 za ukutani na mezani na kusambazwa kwenye Taasisi za Serikali na kwa Wananchi kupitia Masheha na kwenye mikutano ya hadhara. Uchapishaji wa kalenda unatumika kutoa ujumbe kwa Wananchi kwa njia ya picha na maelezo mafupi.

Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi

42. **Mheshimiwa Spika,** matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika kwa ushiriki wa Zanzibar katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa na kuhakikisha kuwa Zanzibar inanufaika na Uhusiano huo. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. 504.5 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 iliingiziwa TZS. 313.2 milioni sawa na asilimia 62 kwa kazi za kawaida.

43. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu hii mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuimarika kwa ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya za Kikanda ikiwemo EAC, SADC, IORA na Tripartite Forum (COMESA, EAC na SADC). Aidha, uhusiano kati ya Serikali na Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi umeongezeka baada ya kuandaliwa Kongamano la Tatu la Watanzania wanaoishi Nje ya Nchi.

44. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano wa kilele wa dharura wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulifanyika Dar es Salaam tarehe 8 Septemba, 2016. Mkutano huo ulihudhuriwa na Mheshimiwa Dk. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Mwenyekiti wa Mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi. Wengine waliohudhuria ni Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda; Mheshimiwa Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda; Mheshimiwa Dk. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa William Rutto, Naibu Rais wa Jamhuri ya Kenya; Mheshimiwa Balozi Alain Aimè Nyamitwe, Waziri wa Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa aliemuwakilisha Mheshimiwa Piere Nkurunziza,

Rais wa Jamhuri ya Burundi; Mheshimiwa Aggrey Tisa Sabuni, Mwakilishi Maalum wa Mheshimiwa Gen. Salva Kiir Mayardit, Rais wa Jamhuri ya Sudan Kusini.

45. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano huo ulipokea taarifa ya majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Ulaya (EPA). Matokeo ya Majadiliano ya Mkutano huo ni kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisisitiza kuwa Mkataba huo utakuwa na athari katika kuimarisha na kulinda viwanda vya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walikubaliana kuwa Nchi Wanachama zipewe muda zaidi wa kutafakari athari za Mkataba huo.

46. **Mheshimiwa Spika,** katika Mkutano huo wa kilele, Jamhuri ya Sudani ya Kusini iliridhia Mkataba wa kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki (Instrument of Ratification of Accession Treaty). Vile vile, mkutano huo ulipokea taarifa ya mafanikio ya mazungumzo ya amani ya Burundi ambapo Mpatanishi wake ni Mheshimiwa Benjamin W. Mkapa, Rais mstaafu wa awamu ya tatu wa Tanzania. Aidha, Mkutano huo ulimteua na kumuapisha Bw. Christophe Bazivamo kutoka Rwanda kushika nafasi ya Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kipindi cha miaka mitatu (3).

47. **Mheshimiwa Spika,** Mikutano mengine ya Kamati za Wataalamu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ilifanyika kati ya mwezi wa Juni, 2016 na mwezi Februari, 2017 katika Miji ya Kampala Uganda, Dar es Salaam na Arusha Tanzania na Nairobi Kenya. Mikutano hiyo ilijadili kiujumla utekelezaji wa Itifaki ya Soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki na uondoshwaji wa vikwazo visivyokuwa vya

kiushuru kwa Nchi Wanachama. Lengo kuu ni kuzifanya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa na mazingira mazuri ya kufanya biashara kwa Maendeleo ya Biashara na Wananchi kwa ujumla.

48. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Arusha mwezi Aprili, 2017. Mkutano huo ulikabidhi rasmi Uenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Jamhuri ya Uganda. Awali Uenyekiti huo ulikuwa unashikiliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hatua za Makabidhiano katika ngazi zote zimekamilika isipokuwa katika ngazi ya Marais ambapo inategemewa baadae mwaka huu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John P. Joseph Magufuli atamkabidhi Uenyekiti huo Rais wa Jamhuri ya Uganda Mheshimiwa Yoweri K. Museveni.

49. **Mheshimiwa Spika,** Mambo mengine yaliyojadiliwa katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri ni pamoja na kuanza rasmi kutumika pasipoti ya kusafiria ya Kimataifa ya kielektroniki ya Afrika Mashariki kuanzia mwezi Januari, 2018. Utaratibu huu ulichelewa kutokana na kwamba Nchi Wanachama kutokuwa tayari katika miundombinu yake. Awali utekelezaji wa zoezi hili ulipangwa kufanyika mwezi Januari, 2017. Vile vile, Mkutano wa Baraza la Mawaziri ulizungumzia kuhusu Ukarabati Mkubwa wa Majengo ya Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili yaliyopo Zanzibar.

50. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano huo uliridhia kuanzishwa kwa Sera ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kufanyika kwa Mkutano mkubwa wa Kiswahili wa Kimataifa Zanzibar mwezi Agosti, 2017. Katika mkutano huo kwa upande wa Zanzibar, iliwakilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Mheshimiwa Issa Haji Ussi Gavu na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman.

51. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi imeendelea kuwajengea uwezo wa uelewa Wananchi na makundi mbali mbali kuhusu fursa zinazopatikana katika Mtangamano wa Jumuiya za Kikanda kama EAC, SADC na IORA. Mafunzo hayo yametolewa kwa Masheha wa Mikoa yote ya Zanzibar, wajasiriamali wa Mikoa minne ikiwemo Mkoa wa Mjini Magharibi, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mkoa wa Kusini Pemba na Mkoa wa Kaskazini Pemba. Aidha, Idara imekaa na Taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kukubaliana kuwa kila Wizara iteue Mwakilishi kiungo kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Mtangamano wa Jumuiya za Kikanda.

52. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano wa kwanza wa kila miaka miwili wa mashirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Afrika Kusini (BI-NATIONAL COMMISSION) ulifanyika kuanzia tarehe 8 Mei, 2017 hadi tarehe 11 Mei, 2017 Jijini Dar es Salaam. Mkutano huo uliambatana na ziara rasmi ya Kitaifa aliofanya Mheshimiwa Jacob Zuma Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini Nchini Tanzania kufuatia mualiko wa Mheshimiwa Dk. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

53. **Mheshimiwa Spika,** katika Mkutano huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Afrika ya Kusini zilikubaliana kuendeleza mashirikiano katika Nyanja za Siasa na Diplomasia, Ulinzi na Usalama, Uchumi na mwisho masuala ya Kijamii na Utamaduni. Zanzibar ilishiriki

kwenye Mkutano huo na kuainisha maeneo kadhaa ya Mashirikiano ikiwemo Mabadiliko ya tabia ya Nchi, Nishati mbadala, Elimu pamoja na Utalii. Makubaliano ya mkutano huo yatafatiwa na kusainiwa kwa Mikataba ya Makubaliano (MOU) hapo baadae. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliiwakilisha Zanzibar katika Mkutano huo.

54. **Mheshimiwa Spika,** kama tulivyoahidi kwamba Serikali itahakikisha inatayarisha Sera ya Diaspora ili kutoa miongozo ya kushughulikia mambo yanayowahusu Wanadiaspora. Naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa Sera hiyo hivi sasa imeshajadiliwa katika Vikao vya Serikali na inatarajiwa kuanza rasmi kutumika katika mwaka wa fedha 2017/2018. Hatua inayofuata ni kutayarisha Mpango Kazi wa miaka mitatu ili kufanikisha utekelezaji wake. Hivi karibuni tutaanza kuwaelimisha Wananchi na makundi mbali mbali kuhusu Sera hiyo.

55. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Idara ya Diaspora imefanikiwa kuandaa Kongamano la Tatu la Watanzania Wanaoishi Nje ya Nchi tarehe 24 hadi tarehe 25 Agosti, 2016 lililofanyika Zanzibar. Kongamano hilo lilihudhuriwa na jumla ya watu 450 wakiwemo Wanadiaspora 300 kutoka Mataifa mbali mbali duniani, Taasisi za Kimataifa, Mabalozi, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Wafanyabiashara. Kaulimbiu ya Kongamano hilo ilikuwa ni “Mtu Kwao Ndio Ngao” na dhamira yake ni kuweka mtazamo mpya wa kuunganisha Utalii na Uwekezaji wa Tanzania kwa Wanadiaspora.

56. **Mheshimiwa Spika,** Kongamano hilo lilifunguliwa na Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kufungwa na Mheshimiwa Januari Yusuph Makamba Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Rais Muungano na Mazingira kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Katika hotuba yake, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliwataka Wanadiaspora kutumia fursa nyingi za Kiuchumi na Kijamii zilizopo Zanzibar na Tanzania kwa ujumla ili kuinua hali ya Uchumi wa Nchi. Alisisitiza Wanadiaspora kuwashawishi Wawekezaji katika Nchi wanazoishi kuja kuwekeza Nchini.

57. **Mheshimiwa Spika,** mada mbali mbali zilijadiliwa katika Kongamano hilo ambazo zililenga kuwajengea uelewa Wanadiaspora kuhusu umuhimu wao katika kuchangia shughuli za Kiuchumi na Kijamii. Vile vile, Wanadiaspora walitakiwa wazifahamu fursa za uwekezaji na utalii zilizopo zitakazoifanya Tanzania iwe Nchi ya Viwanda. Kongamano hilo liliwataka Wanadiaspora kujua wajibu wao wa kuitangaza vizuri Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nje ya Nchi. Aidha, Wanadiaspora walipata fursa ya kuziona bidhaa mbali mbali zinazozalishwa Tanzania kupitia Maonesho ya kibiashara yaliyokuweko kwenye Kongamano hilo. Kadhalika, walipata fursa ya kutembelea Miradi ya Maendeleo na Uwekezaji pamoja na vivutio vya Utalii vilivyopo Zanzibar.

58. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine, Wanadiaspora wa Zanzibar wameendelea kuchangia na kusaidia katika shughuli mbali mbali za kimaendeleo. Katika kipindi cha Julai – Machi, 2016/2017 Wanadiaspora wanaoishi Nchini Seattle Marekani wamesaidia kukusanya viti 562

na meza 500 za kusomea ambazo baadae Serikali ilitoa fedha za kusafirisha kuja Nchini. Vifaa hivyo vimesambazwa katika Skuli ya Sekondari ya Lumumba, Tumekuja na Mwanakwerekwe C kwa Unguja na Fidel Castro na Madungu kwa Pemba. Aidha, Wanadiaspora wa Uingereza wametoa vitabu 100 vya aina mbali mbali kwa Maktaba Kuu ya Zanzibar na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Kwa upande wa sekta ya Afya Wanadiaspora wa Canada wametoa baskeli za magurudumu matatu kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

59. Mheshimiwa Spika, kwa upande mwengine Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi imeendelea kutoa elimu ya kuwafahamisha Wananchi kuhusu suala la Diaspora na umuhimu wa kuwashirikisha Wanadiaspora katika maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii ya Zanzibar. Elimu hiyo ilitolewa kwa Masheha wa Mikoa yote mitano, Maofisa Mipango wa Wilaya, Wajasiriamali, Maofisa Uhamiaji na Waandishi wa Habari Unguja na Pemba.

Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu

60. Mheshimiwa Spika, Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika kwa Mazingira ya Utendaji kazi katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Programu hii inalenga kuimarisha uwezo wa Kiutendaji na Kuratibu Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Unguja na Pemba. Aidha, inalenga Kuimarisha Shughuli za Mipango, Sera na kufanya Utafiti. Kuimarisha shughuli za Usalama wa Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. 2,126.3 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida, na hadi kufikia mwezi Machi, 2017 iliingiziwa TZS. 1,647.3 milioni sawa na asilimia 77 kwa kazi za kawaida.

61. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana kupitia Programu hii ni kuwepo kwa daftari la mahudhurio ya watumishi kwa mfumo wa elektroniki (Biometrics); ambalo litasaidia kudhibiti uingiaji na utokaji kazini. Kuimarika kwa utunzaji wa siri za Serikali kupitia upekuzi unaofanyika kwa Wafanyakazi kabla na baada ya kuajiriwa; kuwepo kwa Ripoti ya Utafiti juu ya Mapitio ya Mpango Mkakati wa Mawasiliano Ikulu pamoja na kuwepo kwa mazingira salama ya kufanyia kazi kupitia ukaguzi wa Majengo ya Serikali unaofanyika mara kwa mara.

62. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeimarisha mazingira ya kazi kwa kusimamia ipasavyo upatikanaji wa huduma na vitendea kazi pamoja na matengenezo ya vyombo vya usafiri. Sambamba na hayo, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imehakikisha kwamba wafanyakazi wote wamelipwa mishahara na stahiki nyengine za watumishi ikiwemo likizo kwa watumishi 46, malipo baada ya saa za kazi watumishi 16 na kuwapatia sare watumishi 36.

63. **Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza ujuzi na maarifa kwa watumishi, Idara imewajengea uwezo watumishi 20 wa kada tofauti ndani na nje ya Nchi katika nyanja za Sayansi ya Jamii, Usimamizi na Ukarimu, Ununuzi na Ugavi, Takwimu na Siasa ya Jamii katika ngazi za cheti, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamivu (kiambatisho Nam. 4 kinatoa ufafanuzi).

64. **Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Uongozi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imekutana mara tatu kujadili mambo mbali mbali yakiwemo utaratibu wa uendeshaji wa Ofisi. Aidha, Kamati Tendaji imefanya vikao vyake kila wiki kwa ajili ya kupata taarifa za usimamizi

wa shughuli za kila siku za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kadhalika, vikao vinne vya Bodi ya Zabuni vimefanyika ambavyo vimejadili ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa mujibu wa Sheria. Vile vile, Kamati vya Ukaguzi wa ndani imefanya vikao vyake kwa ajili ya kupitia utaratibu wa matumizi na kumshauri Katibu Mkuu njia bora za kuimarisha usimamizi wa matumizi.

65. **Mheshimiwa Spika,** Uongozi wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ukiongozwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi umefanya vikao vya wafanyakazi wote wa Unguja, Pemba na Dar es Salaam kwa nyakati tofauti. Vikao hivyo vilijadili utendaji na changamoto zinazojitokeza katika mazingira ya kazi na hatimae kupatiwa ufumbuzi. Matokeo ya vikao hivyo, yameimarisha utendaji na utekelezaji wa Sheria na Mipango ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

66. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanya Mapitio ya Mpango Mkakati wa Idara ya Mawasiliano ya Ikulu. Mapitio hayo yalihusisha kufanya utafiti wa kuangalia namna gani Wananchi wanavyoweza kupata taarifa zinazotolewa na Idara ya Mawasiliano na Habari ya Ikulu. Matokeo ya utafiti huo yataiwezesha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufanya Mapitio ya Mikakati iliyopo na kuweka utaratibu wa kupeleka taarifa kwa Wananchi kirahisi na kufahamu muitikio wao juu ya taarifa hizo. Aidha, Idara imefanya Utafiti juu ya Utoaji wa Huduma kwa Wananchi katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Utafiti huo utapelekea kuwepo kwa Mkataba wa Huduma kwa Wananchi ambao utawawezesha wafanyakazi kutoa huduma bora na kwa wakati kwa Wananchi.

67. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai – Machi 2016/2017, Idara imefuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za (OR) na MBLM. Aidha, Ripoti za utekelezaji za kila robo mwaka, miezi tisa na Ripoti ya Tathmini ya Utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zimeandaliwa. Vile vile, Idara imewezesha kusimamia usalama wa mtandao wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweka vizuizi vya kufanya Kompyuta zisiathiriwe na virusi (Fire walls).

68. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Pemba imesimamia upatikanaji wa huduma na utekelezaji wa shughuli zake kisiwani Pemba. Ofisi hii imeendelea kutekeleza jukumu lake la utunzaji na uendeshaji wa majengo ya Ikulu ya Mkoani na Chake Chake. Aidha, imesimamia ujenzi wa nyumba za Ikulu za Chake Chake na Micheweni. Kwa upande mwengine, Ofisi imeendesha vikao tisa vya Maofisa Wadhamini vilivyoratibu shughuli za kikazi zikiwemo ziara za Mheshimiwa Rais na utambulisho wa Maofisa Wadhamini wapya. Vile vile, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba imesimamia upatikanaji wa mishahara kwa wafanyakazi wake na kuwapatia stahiki nyengine ikiwemo likizo na malipo baada ya saa za kazi.

69. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Usalama wa Serikali imefanya upekuzi wa awali na endelevu kwa watumishi 867 kutoka katika Wizara/Taasisi za Serikali (Kiambatisho Nam. 7 kinatoa ufafanuzi). Aidha, Ofisi imefanya ukaguzi wa kiusalama katika majengo na miundombinu ya Serikali ikiwemo Ofisi za Mamlaka ya Usafiri Baharini (Zanzibar Maritime Authority) Unguja na Pemba na Bohari Kuu ya Madawa Maruhubi. Vile vile, Ofisi imetoa mafunzo juu ya

Utunzaji na Udhibiti wa Siri za Serikali kwa Watumishi 56 wanaotegemewa kuajiriwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (OMPR), Wakurugenzi Utumishi na Uendeshaji 13 wa Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Maofisa 93 wa Idara ya Uhamiaji Unguja na Pemba.

Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu

70. **Mheshimiwa Spika,** matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika Sheria, Sera na Miongozo yenye kusaidia ukuaji wa uchumi, maendeleo ya Nchi na kudumisha amani na mshikamano Nchini. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii iliidhinishiwa TZS 176.5 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 tayari iliingiziwa TZS. 137.5 milioni sawa na asilimia 77.9 kwa kazi za kawaida.

71. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu hii, mafanikio makuu yaliyopatikana ni pamoja na kuiwezesha Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kuratibu kwa ufanisi Mikutano na Vikao vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake. Lengo kuu la kufanyika kwa Mikutano na Vikao hivi ni kuiwezesha Serikali kuwa na mfumo madhubuti wa utendaji wenye kuzingatia Katiba, Sera, Sheria na Kanuni.

72. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imeratibu na kusimamia Vikao vya kawaida na dharura vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake, pamoja na Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu. Katika vikao hivyo, pamoja na mambo mengine, vile vile zilijadiliwa nyaraka zinazohusu Sheria na Sera na kutolewa maamuzi. Aidha, Vikao baina ya Mheshimiwa Rais na Viongozi wa ngazi za juu wa Wizara za SMZ kujadili utekelezaji wa Mipango kazi vilifanyika.

Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi alifanya vikao maalum vya kutathmini na kuhimiza Uwajibikaji wa Watumishi wa Umma katika kutekeleza na kusimamia vyema majukumu na dhamana katika Taasisi zao. (Kiambatisho Nam. 6 kinaonesha nyaraka za Sera na Sheria zilizojadiliwa na Baraza la Mapinduzi).

73. **Mheshimiwa Spika,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein aliongoza semina mbili za kuwajengea uwezo Viongozi wa Kisiasa na Kiutendaji wa Serikali. Semina ya kwanza ilibeba maudhui ya "Umuhimu wa Takwimu, Uzalishaji wake na Matumizi yake". Aidha, semina ya pili ilikuwa na maudhui ya "Umuhimu wa Vyombo vya Habari vya Serikali kwa Maendeleo ya Nchi". Semina hizi mbili zililenga kuhakikisha kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapanga mipango yake kwa kuzingatia matumizi ya takwimu sahihi na kutoa umuhimu kwa Vyombo vya Habari katika kutangaza shughuli za maendeleo.

74. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwa kushirikiana na Taasisi ya UONGOZI ya Dar es Salaam (UONGOZI Institute) iliandaa mafunzo ya siku tatu kwa Makatibu Wakuu kuhusu "Result-Based Management" na "Risk Management and Internal Control System". Aidha, mafunzo mengine ya muda wa siku nne yalitolewa kwa Wakurugenzi Mipango, Sera na Utafiti, Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi na Maofisa Wadhamini kuhusu "Analytical Skills and Strategic Communication" na "Result-Based Management".

75. **Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka wa fedha unaomaliza kuwa Nchi yetu ni Mwanachama wa Mtandao wa Sekretarieti za Mabaraza ya

Mawaziri kwa Nchi za Afrika (Africa Cabinet Government Network – ACGN). Kwa mara ya kwanza Zanzibar imepata heshima ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa nne wa Mtandao huo. Wajumbe kutoka Nchi 13 zilishiriki katika mafunzo ya wiki moja yaliyoendeshwa na wakufunzi kutoka Australia na Uingereza. Nchi hizo ni pamoja na Zanzibar, Tanzania Bara, Botswana, Ghana, Kenya, Lesthoto, Liberia, Malawi, Sierra Leone, Somali, Somaliland, Sudani ya Kusini na Uganda. Nilipata bahati ya kuufungua mkutano huo na nilisisitiza umuhimu wa mashirikiano ya Sekretarieti za Mabaraza ya Mawaziri ili kujenga uwezo na kubadilishana uzoefu.

76. Mheshimiwa Spika, mafanikio makubwa yamepatikana kwa Zanzibar kutokana na kuwa mwenyeji wa Mkutano huu ikiwemo Sekretarieti yetu ya Baraza la Mapinduzi kujifunza katika uandaaji na uchambuzi wa nyaraka za Baraza la Mapinduzi na Kamati zake. Vile vile, Zanzibar imepata fursa nzuri ya kuvitangaza vivutio vya Utalii na Utamaduni wake Kimataifa. Mkutano huo ulifungwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Dk. Abdulhamid Yahya Mzee.

Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi

77. Mheshimiwa Spika, matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika kwa mfumo wa uendeshaji wa shughuli za Ofisi, uhifadhi wa nyaraka, mazingira ya kazi, kuongeza ufanisi na uwajibikaji kazini. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii iliidhinishiwa TZS. 1,315.5 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii na hadi kufikia mwezi Machi, 2017 tayari iliingiziwa TZS. 842.7 milioni sawa na asilimia 64.1kwa kazi za kawaida.

78. Mheshimiwa Spika, utendaji wa watumishi umeendelea kuimarika na kuwa wenye ufanisi na tija zaidi kutokana na kuweka mazingira mazuri na vitendea kazi pamoja na kuendeleza programu za kujenga uwezo wa kitaaluma kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kulingana na mahitaji na mabadiliko ya wakati. Jumla ya watumishi wanne wanaendelea kupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za Stashahada (Utunzaji wa Kumbukumbu), Shahada (Sayansi ya Habari) na Shahada ya Uzamili wafanyakazi wawili (Utafiti katika Sera za Umma na Sayansi ya Kompyuta). Watumishi wengine wanane wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi sambamba na kutoa taaluma ya namna bora ya kujikinga na maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI. Kadhalika, Ofisi imesimamia ulipaji wa mishahara na stahiki nyengine kwa wakati ikiwemo likizo kwa wafanyakazi na sare kwa watumishi.

3. MWELEKEO WA BAJETI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

79. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeandaa bajeti yake ya mwaka wa fedha 2017/2018 kwa mujibu wa miongozo ya Serikali pamoja na kutayarisha maelezo ya bajeti inayotumia mfumo wa "Program Based Budget". Katika kutekeleza bajeti hii, jumla ya Program Kuu 5 na Programu Ndogo 11 zimeandaliwa. Mwelekeo wa bajeti hii umezingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo MKUZA, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya 2015 – 2020, Maelekezo na Miongozo inayotolewa na Viongozi wetu pamoja na miongozo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

80. **Mheshimiwa Spika,** naomba kulihakikishia Baraza lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maelekezo na miongozo madhubuti ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba imeiandaa. Lengo ni kuhakikisha kuwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inatoa mchango mkubwa katika kuiwezesha Zanzibar kupiga hatua za kimaendeleo.

81. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 imejipangia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Rais, Baraza la Mapinduzi na Kamati zake;
ii. Kusimamia utekelezaji wa kazi za Baraza la Mapinduzi, Kamati zake na Kamati ya Makatibu Wakuu kwa kuzingatia Katiba na Sheria za Nchi;
iii. Kuwahudumia Wananchi kwa kuzitekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais, pamoja na kuwapatia taarifa za shughuli za Serikali na maendeleo ambayo ni haki yao ya Kikatiba;
iv. Kusimamia utendaji, ufanisi na kufanikisha kazi katika (OR) na MBLM;
v. Kuendeleza ujenzi na kuimarisha usalama wa nyumba za Ikulu; na
vi. Kusimamia maendeleo ya wafanyakazi wa (OR) na MBLM katika kutekelza wajibu wao, uendelezaji wa maslahi yao, stahiki na haki zao ili wawatumikie Wananchi ipasavyo.

82. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na vipaumbele vilivyopangwa, Ofisi inategemea kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
ii. Kuratibu Vikao vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake pamoja na Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu;
iii. Kutathmini utekelezaji wa shughuli za kila siku za (OR) na MBLM, Idara na Taasisi pamoja na maamuzi ya Serikali;
iv. Kuwajengea uwezo Watendaji ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi;
v. Kuwawezesha Wananchi kupata taarifa juu ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali yao kupitia Jarida na vipindi vya redio;
vi. Kuwawezesha Watendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushiriki katika majadiliano ya Jumuiya za Kikanda yenye kuleta tija kwa Zanzibar;
vii. Kuwashajihisha Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi kuchangia katika maendeleo ya Zanzibar;
viii. Kuimarisha upatikanaji wa takwimu katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na
ix. Kukusanya na kufuatilia utekelezaji wa Sera, Sheria na Miongozo yote ya Serikali.

3.1 PROGRAMU KUBWA NA NDOGO NA MAKISIO YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

83. Mheshimiwa Spika, Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zitatekelezwa na Ofisi na Idara zifuatazo:-

i. Ofisi ya Faragha ya Rais;
ii. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi;
iii. Idara ya Huduma za Rais;
iv. Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu;

v. Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi;
vi. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
vii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
viii. Ofisi ya Usalama wa Serikali; na
ix. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi –Pemba.

84. **Mheshimiwa Spika,** Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Fungu A01 ni kama zifuatazo:-

1. Programu ya Kusimamia Huduma na Shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu

85. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni kusimamia huduma na Shughuli za Mheshimiwa Rais na kuendeleza Taswira nzuri kwa Umma. Aidha, kuendeleza Taswira nzuri ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni Umma na Wananchi wote kwa jumla kuwa na uelewa kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Mheshimiwa Rais. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Kusimamia Huduma na Shughuli za Mheshimiwa Rais; na
ii. Programu Ndogo ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi.

86. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii itatekelezwa sambamba na Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali za Ikulu (State Lodges).

87. Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kufuatilia ahadi na maagizo ya Mheshimiwa Rais;
ii. Kuratibu ziara za ndani na za nje za Mheshimiwa Rais;
iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi;
iv. Kulipa mishahara ya wafanyakazi na stahiki nyengine;
v. Kukuza mawasiliano baina ya Mheshimiwa Rais na Wananchi;
vi. Kutayarisha, Kuchapisha na Kusambaza machapisho; na
vii. Kuimarisha tovuti ya (OR) na MBLM.

88. Mheshimiwa Spika, shughuli nyengine zitakazotekelezwa ni:-

i. Kuendelea na ujenzi wa Ikulu ndogo ya Micheweni;
ii. Kufanya matengenezo katika Ikulu ndogo ya Laibon;
iii. Kufanya matengenezo katika Ikulu ndogo ya Dodoma;
iv. Kufanya matengenezo katika Ikulu ya Mnazi Mmoja;
v. Kuzuwia mmong'onyoko katika Ikulu ndogo ya Migombani; na
vi. Kufanya matengenezo katika Ikulu ndogo ya Bwefum.

89. Mheshimiwa Spika, ili Programu ya Kusimamia Shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 3,664.1 milioni. Kati ya hizo TZS. 2,934.1 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS. 730.0 milioni kwa kazi za maendeleo.

2. Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi

90. Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha mashirikiano na Jumuiya za Kikanda, Kimataifa na Kuwashirikisha ipasavyo Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi katika maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii ya Zanzibar. Aidha, matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni Zanzibar kufaidika na fursa za Kiuchumi na Kijamii zinazotokana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kikanda na Kimataifa; na
ii. Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi.

91. Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuendesha vikao vya ndani vya mashauriano vya kisekta;
ii. Kushiriki katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa ndani na Nje ya Nchi;
iii. Kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa Mtangamano wa Jumuiya za Kikanda na dhana ya Diaspora na umuhimu wake kwa maendeleo ya jamii;
iv. Kutekeleza Mpango Kazi wa Sera ya Diaspora; na
v. Kuandaa Kongamano la Watanzania wanaoishi Nje ya Nchi.

92. Mheshimiwa Spika, ili Programu ya Ofisi ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. TZS. 508.1 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

3. Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu

93. Mheshimiwa Spika, malengo makuu ya Programu hii ni kuimarisha uwezo wa kiutendaji na kuratibu shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu; Kuimarisha Shughuli za Mipango, Kuandaa na Kuchambua Sera na Kufanya Utafiti; Kuimarisha Shughuli za Upekuzi kwa Watumishi kabla na baada ya Kuajiriwa na Kuimarisha Usalama wa Majengo na Miundombinu ya Serikali. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika kwa mazingira ya utendaji kazi. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo nne zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu;
ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za ORMBLM;
iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za ORMBLM – Pemba; na
iv. Programu Ndogo ya Kusimamia Usalama wa Watumishi wa Umma.

94. Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kulipa mishahara kwa wafanyakazi na stahiki zao;
ii. Kuratibu Database ya Maendeleo ya Rasilimali Watu ya ORMBLM;
iii. Kufanya ukaguzi wa hesabu wa awali na endelevu katika Ofisi;

iv. Kufanya Mapitio ya Ripoti ya Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo na Mpango wa Mafunzo;
v. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu, waajiriwa wapya na taaluma ya kujikinga na majanga ya moto;
vi. Kuendesha Vikao vya Bodi ya zabuni na Kamati za Ukaguzi;
vii. Kukusanya taarifa za utekelezaji wa shughuli za ORMBLM;
viii. Kufanya utafiti juu ya fursa zinazopatikana katika soko la Afrika Mashariki;
ix. Kufanya utafiti wa kuangalia mchango wa Diaspora wa Zanzibar juu ya Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii kwa kushirikiana na Tume ya Mipango ya Zanzibar;
x. Kuratibu na Kuandaa Mikutano ya Mapitio ya PBB na Maandalizi ya Bajeti;
xi. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli za ORMBLM;
xii. Kukusanya, Kuchambua na Kuandaa Ripoti za Takwimu za ORMBLM;
xiii. Kulinda, kuhifadhi na kutoa huduma kwa Ikulu na Nyumba za Serikali zilizoko Pemba;
xiv. Kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za ORMBLM Pemba;
xv. Kufanya upekuzi wa awali wa kiusalama na endelevu kwa wafanyakazi;
xvi. Kufanya ukaguzi wa kiusalama katika majengo na miundombinu ya Serikali; na
xvii. Kutoa mafunzo kwa watumishi juu ya utunzaji wa siri na maadili ya kazi.

95. Mheshimiwa Spika, ili Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi Rais Ikulu iweze kutekelezwa, kwa

mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. TZS. 2,462.2 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.

96. **Mheshimiwa Spika,** Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Fungu A02 ni hizi zifuatazo:-

1. Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu

97. **Mheshimiwa Spika,** lengo la Programu hii ni kuhakikisha uwajibikaji wa Serikali katika Kutoa huduma kwa Wananchi. Aidha, kuhakikisha malengo ya Wizara na Taasisi za Serikali yanatekelezwa ipasavyo na kufikiwa. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika Sera, Sheria na Miongozo yenye kusaidia ukuaji wa uchumi, maendeleo na kudumisha amani na umoja Nchini. Program hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia shughuli za Baraza la Mapinduzi na Kamati zake; na
ii. Programu Ndogo ya Tathmini ya Utendaji kazi na Uwajibikaji wa Taasisi za Umma.

98. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kutayarisha vikao vya kawaida na dharura vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake ikiwemo Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu;

ii. Kutoa mafunzo ya kujenga uwezo na miongozo ya kazi kwa watendaji wakuu wa Serikali na Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi;
iii. Kuandaa vikao baina ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Viongozi wa Wizara za SMZ kutathmini utekelezaji wa Mipango kazi ya Wizara na Taasisi za SMZ;
iv. Kuandaa vikao baina ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi na Viongozi wa Wizara za SMZ ili kuhimiza Ufanisi na Uwajibikaji wa Watumishi wa Umma;
v. Kuimarisha Uhusiano na ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya na Majukwaa ya Kikanda na Kimataifa;
vi. Kufuatilia na Kufanya Tathmini ya Utekelezaji wa Maamuzi, Miongozo, Sera na Sheria zinazotekelezwa na Serikali na Taasisi zake; na
vii. Kufuatilia na kuimarisha hali ya Utumishi wa Umma Nchini.

99. Mheshimiwa Spika, ili Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu iweze kutekelezwa kikamilifu, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 394.0 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.

2. Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi

100. Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha mazingira ya kazi, mahusiano ya Umma na kuongeza ujuzi wa Wafanyakazi. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuwa na mfumo bora na wa kisasa wa

kuendesha shughuli za Ofisi na Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo moja ifuatayo:-

i. Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

101. Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuimarisha miundombinu ya Ofisi, majengo pamoja na mazingira yake;
ii. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano na utekelezaji wa kazi za kila siku za kiofisi;
iii. Kufuatilia na kutekeleza shughuli muhimu za kikazi ndani ya Nchi;
iv. Kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi wa ofisi;
v. Kutoa mafunzo ya kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI;
vi. Kuimarisha Huduma za Maktaba na Kitengo cha uandaaji, usambazaji, uhifadhi na utunzaji wa kumbukumbu za Baraza la Mapinduzi; na
vii. Kuongeza ari, bidii na tija ya kazi kwa wafanyakazi.

102. Mheshimiwa Spika, ili Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iweze kutekelezwa kikamilifu, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 1,313.9 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

4. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

4.1 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MRADI WA MAENDELEO

103. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2017/18, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inakadiria kutumia jumla ya TZS. 8,342.6 milioni kwa ajili ya Matumizi ya utekelezaji wa Programu za Fungu A01 na A02. Fungu A01 linakadiriwa kutumia TZS. 6,634.7 milioni kwa kazi za kawaida na mradi wa maendeleo. Kati ya fedha hizo, TZS. 5,904.7 milioni kwa ajili ya kazi za kawaida na TZS. 730.0 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maendeleo. Fungu A02 linakadiriwa kutumia TZS. 1,707.9 milioni kwa kazi za kawaida.

4.2 MAOMBI YA FEDHA 2017/2018

104. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka 2017/2018, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makadirio ya matumizi ya Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zenye jumla ya TZS. 8,342.6 milioni. Kati ya fedha hizo, TZS. 7,612.6 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TZS. 730.0 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wa fedha zitakazotumika kwa utekelezaji wa kila Programu zimeainishwa katika Kiambatisho Namba 2.

5. HITIMISHO

105. Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha hotuba yangu, naomba nimshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein kwa namna anavyotekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Utekelezaji wake wa ahadi unawapa faraja na matumaini Wananchi katika ustawi wa maendeleo yao. Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie maisha marefu na aendelee kumpa afya njema ili aendelee kutuongoza na kutuletea neema Wazanzibari.

106. Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize kuhusu suala muhimu la kudumisha amani na utulivu kwani ndio nguzo ya maendeleo yetu. Aidha, naendelea kutoa wito kuwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukiwa Wawakilishi wa Wananchi ni wajibu wetu kuwa mstari wa mbele kuhubiri amani na kutekeleza kwa vitendo katika kuzisimamia shughuli za Wananchi na tuzitekeleze ahadi tulizozitoa wakati wa kuomba ridhaa Majimboni kwetu.

107. Mheshimiwa Spika, kwa mara nyengine, nachukua fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe Mheshimiwa Spika kwa namna unavyokiongoza chombo hiki chenye nafasi na heshima kubwa kwa Nchi yetu. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa namna mlivyokuwa watulivu wakati nawasilisha hotuba yangu. Ni matumaini yangu kuwa mtatoa michango mizuri na ushauri kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambayo itasaidia katika utekelezaji wa majukumu yetu.

108. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee ninawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza

la Mapinduzi kwa mchango wao mkubwa walionipa na kushirikiana nami katika kutekeleza majukumu mbali mbali ya Ofisi hii. Kwanza, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee; Washauri wa Mheshimiwa Rais; Naibu Makatibu wa Baraza la Mapinduzi, Ndugu Salmin Amour Abdalla na Dkt. Juma Yakuti Juma wanastahiki pongezi maalum kwa uwajibikaji wao mkubwa wenye kupigiwa mfano. Nawashukuru pia Katibu Mkuu Ndugu Salum Maulid Salum, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Rahma Ali Khamis, Katibu wa Rais Ndugu Haroub Shaib Mussa na Naibu wake Ndugu Maryam Haji Mrisho, Mkurugenzi wa Huduma za Rais Ikulu na Wasaidizi wote wa Mheshimiwa Rais; Ofisa Mdhamini ORMBLM - Pemba, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ujumla wao.

109. Mheshimiwa Spika, naliomba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na kuipitisha Bajeti hii sambamba na kutupatia ushauri na maelekezo ambayo yataimarisha utekelezaji wake.

110. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

(Mheshimiwa Issa Haji Ussi Gavu)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

KIAMBATISHO 1: ORODHA YA WAGENI WALIOFIKA IKULU KUONANA NA MHESHIMIWA RAIS

TAREHE	JINA LA MGENI
11.07.2016	Bwana Kunal Kapoor, Mkongwe wa Filamu za Kihindi, kutoka nchini India.
12.07.2016	Mheshimiwa Mohamed Haji Hamza, Balozi wa Tanzania nchini Misri.
20.08.2016	Madaktari Bingwa kutoka Hospitali ya Chuo Kikuu cha El-Shatby kiliopo Alexandria nchini Misri.
23.08.2016	Bwana Mauricio Ramos, Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Millicom Group akifutana na ujumbe wake.
26.08.2016	Mheshimiwa Tek Chand Barupal, Balozi Mdogo wa India aliyepo Zanzibar.
	Mheshimiwa Xie Xiaowu, Balozi Mdogo wa Jamhuri ya Watu wa China alyepo Zanzibar.
07.09.2016	Mheshimiwa Monica Patrice Clemente Mussa, Balozi wa Msumbiji nchini Tanzania
21.09.2016	Bwana Brian Malcom Thomson, Mmiliki wa Mradi wa Penny Royal.
03.10.2016	Mheshimiwa Salvador Antonio Valdes Mesa, Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Cuba.
04.10.2016	Mheshimiwa Hamad Masauni Yussuf, Naibu Waziri wa Mambo ya ndani Tanzania
12.10.2016	Mheshimiwa Dk. Suzan A. Kolimba, Naibu Waziri Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.
30.10.2016	Bwana Yasushi Kanzaki, Makamo wa Rais wa Taasisi ya Mashirikiano ya Kimataifa ya Japan (JICA).
10.11.2016	Bwana Evind Hansen, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chuo Kikuu cha Haukeland nchini Norway.
23.11.2016	Mheshimiwa Hazem Shabat, Balozi wa Palestine nchini Tanzania.
29.11.2016	Bibi Maniza Zamani, Mwakilishi wa UNICEF nchini Tanzania.
	Bibi Francesca Morandini, Mwakilishi wa UNICEF Zanzibar.
	Mheshimiwa Chirau Ali Makwere, Balozi wa Kenya nchini Tanzania.
30.11.2016	Askofu Michael H. Hafidh, Anglican Zanzibar akifuatana na ujumbe wake kutoka Kanisa la Anglican, Zanzibar
21.12.2016	Dk. Tonia Kandiero, Mwakilishi Mkaazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).
27.12.2016	Mheshimiwa Ahmed bin Humood Al - Habsi, Balozi Mdogo wa Oman aliyepo Zanzibar.
27.12.2016	Mheshimiwa Jorge Luis Lopez Tormo, Balozi wa Jamhuri ya Cuba nchini Tanzania.
10.01.2017	Bwana Wooyang Chung, Makamo wa Rais wa KOICA kutoka Korea.
	Bwana Joonsung Park, Mkurugenzi Mkaazi wa KOICA nchini Tanzania.
	Bwana Yoon Suk Myum, Makamo Mwenyekiti wa Seoul Broadcasting System TV ya Korea akifuatana na ujumbe wake kutoka Korea.
	Bwana Kim In Hee, Makamo Mwenyekiti wa Taasisi isiyo ya Kiserikali ya "Good Neighbours International" kutoka Korea akifuatana na ujumbe wake.
13.01.2017	Gen. D. A. Mwamunyange, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama Tanzania.
10.02.2017	Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Balozi wa Tanzania nchini Brazil.
	Mheshimiwa Prof. Elizabeth Kiondo, Balozi wa Tanzania nchini Turkey.
	Mheshimiwa George Madafa, Balozi wa Tanzania nchini Italy.
	Mheshimiwa Lt.Gen.Paul Mella (rtd), Balozi wa Tanzania, DRC.
	Mheshimiwa Dr. James Alex Mseleka, Balozi wa Tanzania, GENEVA (UN).
	Mheshimiwa Samuel Shelukindo, Balozi wa Tanzania nchini Ufaransa.
	Mheshimiwa Mbelwa Kairuki, Balozi wa Tanzania nchini China.
23.02.2017	Mheshimiwa Yuri Popov Fedorovich, Balozi wa Urusi nchini Tanzania.

01.03.2017	Wakurugenzi Watendaji (12) wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) wakiongozwa na Mwenyekiti wao Bibi Elizabeth Lekhethe Mmakgoshi, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa AfDB anayeziwasilisha nchi za Afrika Kusini, Lesotho na Swaziland.
03.03.2017	Mheshimiwa Tan Puay Hiang, Balozi wa Singapore nchini Tanzania.
	Mheshimiwa Pindi Chana, Balozi wa Tanzania nchini Kenya
	Mheshimiwa Abdallah Kilima, Balozi wa Tanzania nchini Oman.
	Mheshimiwa Silima Kombo Haji, Balozi wa Tanzania nchini Sudan.
	Mheshimiwa Joseph E. Sokoine, Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji.
	Mheshimiwa Fatma Rajabu, Balozi wa Tanzania nchini Qatar.
	Mheshimiwa Matilda Swilla Masuka, Balozi wa Tanzania nchini Korea Kusini.
	Mheshimiwa Grace Mgovano, Balozi wa Tanzania nchini Uganda.
14.03.2017	Mheshimiwa Carlos A. Puente, Balozi wa Brazil nchini Tanzania.
15.03.2017	Gen. Vs Mabeyo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Tanzania.
20.03.2017	Dk. Anna Peter Makakala, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Tanzania
23.03.2017	Mheshimiwa Guo Jinlong, Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) na Katibu wa Kamati ya Chama cha Kikomunisti cha Manispaa ya Beijing.
27.03.2017	Dr. Hosea Piquer, Rais wa Taasisi ya Maendeleo ya Elimu inayohusiana na Upasuaji wa Mishipa ya Fahamu, Uti wa Mgongo na Vichwa Maji (NED Foundation) akifuatana na ujumbe wa Wataalmu wa Upasuaji wa Kichwa na Uti wa Mgongo.
11.04.2017	Bwana Alvero Rodriguez, Mratibu Mkaazi wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini Tanzania ambaye pia ni Mwakilishi Mkaazi wa UNDP nchini Tanzania akifuatana na Wawakilishi 23 wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN) nchini Tanzania.
	Prof. Yunus Daud Mgaya, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Maradhi ya Binaadamu.
	Mheshimiwa Sylivester Massele Mabumba, Balozi wa Tanzania nchini Comoro.
	Mheshimiwa Job Daudi Massima, Balozi wa Tanzania nchini Israel.
	Mheshimiwa Dkt. Abdalla Saleh Posi, Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani.
	Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Balozi wa Tanzania nchini Algeria.
	Mheshimiwa Baraka H. Luvanda, Balozi wa Tanzania nchini India.
	Mheshimiwa Sylivester M. Ambukile, Balozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini.
	Bwana Wang Yiwen, Rais wa ZTE Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika akifuatana na ujumbe wake.
19.04.2017	Mheshimiwa Lucas Domingo Hernandez Polledo, Balozi wa Jamhuri ya Cuba nchini Tanzania.
24.04.2017	Mhandisi Amr Hassan Allouba, Mwenyekiti wa Kampuni ya Engineering Consultant Group (ECG) kutoka Misri.

KIAMBATISHO 2: MAPITIO YA UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

JINA LA IDARA	PROGRAMU NDOGO	BAJETI KWA MWAKA WA 2016/2017	FEDHA ZA MIEZI TISA 2016/2017	ASILIMIA YA FEDHA KWA MWAKA
Ofisi ya Faragha ya Rais	Uratibu wa Shughuli za Mheshimiwa Rais	2,167,003,000	1,979,335,857	91
	Uratibu wa Shughuli za Mheshimiwa Rais (Mradi wa Maendeleo)	500,000,000	500,000,000	100
Idara ya Mawasiliano na Habari - Ikulu	Uimarishaji wa Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi	200,351,000	187,036,392	93
Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	Programu Ndogo ya Uratibu wa shughuli za Baraza la Mapinduzi na Kamati zake	109,200,000	102,449,800	94
	Programu Ndogo ya Tathmini ya Utendaji Kazi na Uwajibikaji wa Taasisi za Umma	35,360,000	34,250,000	97
	Ukuzaji ufanisi wa kitengo cha TEHAMA	31,930,000	4,205,060	13
	Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	1,179,210,000	833,971,240	71
	Uimarishaji uwezo wa Ofisi katika kusimamia Sera, Sheria, Utumishi wa Umma na Uhifadhi wa Nyaraka.	136,400,000	30,955,000	23

JINA LA IDARA	PROGRAMU NDOGO	BAJETI KWA MWAKA WA 2016/2017	FEDHA ZA MIEZI TISA 2016/2017	ASILIMIA YA FEDHA KWA MWAKA
Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje	Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi	264,673,000	185,053,950	70
	Uratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala ya Diaspora	239,847,000	128,102,300	53
Idara ya Uendeshaji na Utumishi	Kuratibu na Kusimamia Shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu	1,122,435,000	883,092,750	79
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za ORMBLM	300,778,000	241,404,500	80
Ofisi ya Ofisa Mdhamini - Pemba	Kuratibu na kusimamia shughuli za ORMBLM - Pemba	663,113,000	490,438,298	74
Ofisi ya Usalama wa Serikali (G.S.O)	Usimamizi wa Usalama wa Watumishi wa Umma	40,000,000	32,350,000	81
	Jumla	**6,990,300,000**	**5,632,645,147**	**79**

KIAMBATISHO 3: MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

PROGRAMU/PROGRAMU NDOGO	MSHAHARA	UENDESHAJI OFISI	MATUMIZI YA MAENDELEO	MAPENDEKEZO 2017/2018
Kusimamia shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu	**2,165,251,000**	**768,836,000**	**730,000,000**	**3,664,087,000**
Kusimamia Huduma na Shughuli za Mheshimiwa Rais	2,031,456,000	599,420,000	730,000,000	3,360,876,000
Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi	133,795,000	169,416,000		303,211,000
Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu	**881,900,000**	**826,000,000**	**-**	**1,707,900,000**
Programu Ndogo ya Uratibu wa shughuli za Baraza la Mapinduzi na Kamati zake	881,900,000	139,531,000		139,531,000
Programu Ndogo ya Tathmini ya Utendaji Kazi na uwajibikaji wa Taasisi za Umma		254,499,000		98,084,475
Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi		431,970,000		1,470,284,525
Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi	**136,227,000**	**372,227,000**	**-**	**508,454,000**
Kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kikanda na Kimataifa	136,227,000	170,162,000		306,389,000

PROGRAMU/PROGRAMU NDOGO	MSHAHARA	UENDESHAJI OFISI	MATUMIZI YA MAENDELEO	MAPENDEKEZO 2017/2018
Kuratibu Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi		202,065,000		202,065,000
Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu	**1,428,522,000**	**1,033,637,000**	**-**	**2,462,159,000**
Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu	798,162,000	441,900,000		1,240,062,000
Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za ORMBLM	90,227,000	196,737,000		286,964,000
Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za ORMBLM - Pemba	540,133,000	320,000,000		860,133,000
Kusimamia Usalama wa Watumishi wa Umma		75,000,000		75,000,000
JUMLA KUBWA	**4,611,900,000**	**3,000,700,000**	**730,000,000**	**8,342,600,000**

KIAMBATISHO 4: MAFUNZO YA MUDA MREFU KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2016/2017

NAMBA	NGAZI YA ELIMU	FANI	IDADI YA WAFANYAKAZI	
			ME	KE
1	Shahada ya Uzamivu	Sayansi ya Siasa	1	
		Lugha ya Kiswahili	1	
		Sheria za Kimataifa		1
2	Shahada ya uzamili	Utafiti na Sera za Umma	1	
		Sayansi ya Kompyuta	1	
		Sheria		1
		Uchumi	1	
		Ushirikiano wa Kimataifa na maendeleo	1	
4	Shahada	Utawala wa Biashara	2	
		Utatuzi wa Migogoro		1
		Ustawi wa Jamii		1
		Takwimu		1
		Sayansi ya Habari		1
		Mawasiliano ya Umma		1
		Uhusiano wa Kimataifa		1
5	Stashahada	Utunzaji Kumbukumbu		1
		Ununuzi na Ugavi	1	
6	Cheti	Usimamizi na Ukarimu	3	
	JUMLA		**12**	**9**

KIAMBATISHO 5: IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOENDA LIKIZO KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI, 2016/2017

NA.	JINA LA IDARA/TAASISI	UNGUJA		PEMBA		JUMLA KUU
		MME	MKE	MME	MKE	
1	OFISI YA FARAGHA YA RAIS	20	19			39
2	OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI	6	2			8
3	IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA WAZANZIBARI WANAOISHI NJE YA NCHI	7				7
4	IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	9	9			18
5	IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI	1				1
6	OFISI YA AFISA MDHAMINI OR MBLM PEMBA			1	3	4
	JUMLA KUU	**43**	**30**	**1**	**3**	**77**

KIAMBATISHO 6: ORODHA YA NYARAKA ZA SERA NA SHERIA ZILIZOJADILIWA NA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MAẒHI 2016/2017

NAM	SERA/SHERIA
1.	Sheria ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
2.	Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.
3.	Mapendekezo ya Kutungwa Sheria Mpya ya Fedha za Umma na Kufutwa Sheria Nambari 12/2005.
4.	Mapendekezo ya Kutungwa Sheria Mpya ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali Chakavu za Serikali na Kufutwa Sheria Nambari 9/2005.
5.	Mapendekezo ya Kutungwa kwa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Zanzibar.
6.	Kuridhiwa kwa Sheria Nambari 14/2016 ya Makosa ya Mtandao ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
7.	Mapendekezo ya Marekebisho ya Baadhi ya Vifungu vya Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Nambari 7/2014.
8.	Marekebisho ya 11 ya Katiba ya Zanzibar, 1984.
9.	Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Nambari 2/2006.
10.	Mswada wa Kufutwa na Kutungwa Upya Sheria ya Ushahidi.
11.	Mswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nambari 2 ya mwaka 2005, Kuweka Masharti Bora Zaidi kwa ajili ya Ufanisi na Usimamizi Imara wa Mfuko na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.
12.	Mswada wa Sheria Mpya ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Itakayochukuwa Nafasi ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nambari 9/2005.
13.	Mswada wa Sheria Mpya ya Usimamizi wa Fedha za Umma Itakayochukuwa Nafasi ya Sheria ya Fedha Nambari 12 ya Mwaka 2005.
14.	Mapendekezo ya Kufutwa Sheria Nambari 9 ya Mwaka 1992 na kutungwa Sheria Mpya ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.
15.	Mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria ya Kusimamia Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar.
16.	Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
17.	Sera ya Diaspora ya Zanzibar.
18.	Mapendekezo ya Sera ya Malipo ya Watumishi wa Umma Zanzibar.
19.	Mapendekezo ya Kurekebisha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar, Nambari 4/2015.
20.	Rasimu ya Sheria ya Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara.

KIAMBATISHO 7: IDADI YA WATUMISHI WALIOFANYIWA UPEKUZI NA TAASISI WANAZOTOKA

NA.	JINA LA TAASISI	IDADI YA WAPEKULIWA
1.	Shirika la Umeme Zanzibar	21
2.	Chuo cha Taifa cha Zanzibar	8
3.	Chuo cha Uongozi wa Fedha Zanzibar	4
4.	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa	14
5.	Benki ya Watu ya Zanzibar	55
6.	Shirika la Meli	6
7.	Shirika la Bandari	21
8.	Idara ya Uhamiaji	93
9.	Mahakama	3
10.	Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar	21
11.	Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi	1
12.	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar	7
13.	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	186
14.	Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	60
15.	Baraza la Wawakilishi	13
16.	Shirika la Bima la Zanzibar	8
17.	Wizara ya Afya	302
18.	Baraza la Mji Wete	12
19.	Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	1
20.	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar	24
21.	Shirika la Huduma za Maktaba	7
	Jumla Kuu	**867**